Maelezo ya

# Nyakati saba za kanisa

## Sura ya Kumi

## Resume ya Enzi

Kwa kuwa masomo yetu yamekuwa maelezo ya aya kwa aya ya Maandiko yale yanayohusika na zile nyakati saba, hatujaweka mfululizo wa kielelezo cha kihistoria cha kanisa kama jinsi ambavyo ingelitupasa kufanya. Kwa hiyo, sasa ni kusudi letu, basi, sasa kuchukua sura hii, na tukianzia na Wakati wa Efeso tufuatilie katika nyakati zote kanisa na historia yake kama ilivyopewa Yohana na Roho wa Mungu. Hatutakuwa tukiongezea mambo mapya zaidi ya kuunganisha yale tuliyonayo tayari.

Kutokana na masomo yetu tayari tumejua ya kwamba sehemu kubwa ya Ufunuo inaeleweka vibaya kabisa kwa sababu hatukujua hapo kabla ya kwamba lile 'kanisa' linalonenwa habari zake na linalozungumziwa katika kitabu hiki halihusu 'ekklesia' pekee 'walioteuliwa,' 'mwili wa Kristo,' 'bibi-arusi,' bali yananazungumzia mwili mzima wa watu wanaoitwa Wakristo, kama ni wa kweli ama ni wa jina tu. Kama vile Israeli wote SIYO Israeli, vivyo hivyo Wakristo wote SIYO Wakristo. Kwa hivyo tulijifunza ya kwamba kanisa limeundwa na mizabibu miwili, ile ya kweli na ya uongo. Hiyo mizabibu miwili inaongozwa na roho za aina mbili; mmoja una Roho Mtakatifu wakati huo mwingine umejazwa na roho ya mpinga-Kristo. Yote miwili inadai kumjua na kujulikana na Mungu. Yote miwili inakusudia kunena kwa niaba ya Mungu. Yote miwili inaamini kweli fulani za kimsingi na inatofautiana juu ya nyingine. Lakini kwa kuwa yote miwili ina jina la Bwana, ikiwa ikiitwa Wa-Kristo, na kwa kufanya hivyo ni dhahiri inadai uhusiano Naye (Mungu anaita hilo ndoa), Mungu sasa anawawajibisha yote miwili Kwake na kwa hiyo anazungumza na kila mmoja.

Tulijifunza zaidi ya kwamba mizabibu hii miwili ingekua pamoja mpaka mwisho wa zile nyakati ambapo yote miwili itakomaa na yote kuvunwa. Mzabibu wa uongo usingeshinda na kuuangamiza mzabibu wa kweli, lakini basi, wala mzabibu wa kweli usingeweza kuuleta mzabibu wa uongo katika uhusiano wa wokovu na Yesu Kristo.

Tulijua ukweli wa ajabu sana ya kwamba Roho Mtakatifu angeweza kushuka na angeshuka juu ya Wakristo walio wa mzabibu wa uongo wasiozaliwa mara ya pili na kudhihirika kwa nguvu katika ishara na maajabu mbalimbali, kama tu vile Yuda alivyokuwa na huduma dhahiri katika Roho Mtakatifu ingawa yeye, mwenyewe, alitangazwa kuwa ni ibilisi.

Tukiwa na kanuni hizi mawazoni tunaanza kulifuatilia kanisa katika nyakati mbalimbali saba.

Kuzaliwa kwa kanisa kulifanyika siku ya Pentekoste. Kama vile Adamu wa kwanza alivyopewa bibiarusi moja kwa moja kutoka katika mkono wa Mungu naye alikuwa hajatiwa unajisi kwa kitambo kidogo, vivyo hivyo na Kristo, Adamu wa mwisho, alipewa bibi-arusi msafi na asiyeghoshiwa pale Pentekoste; naye alibaki akiwa ametengwa na hajatiwa unajisi kwa kitambo kidogo.

> *"Na katika wote wengine hapana mtu hata mmoja aliyethubutu kuambatana nao."*

(Matendo 5:13) na

> *"Bwana akalizidisha kanisa kila siku kwa wale waliokuwa wakiokolewa."*

Matendo 2:47.

Ni muda gani jambo hili liliendelea hatujui, lakini siku moja kama vile Hawa alivyojaribiwa na kutongozwa na Shetani, vivyo hivyo kanisa lilitiwa unajisi kwa kuingia kwa roho wa mpinga-Kristo.

> *"Na hii ndiyo roho ya mpinga Kristo ambayo mmesikia kwamba yaja; na sasa imekwisha kuwako duniani."*

Yohana 4:3.

Na Yesu alisema kuhusu bibi-arusi Wake katika ule wakati wa kwanza,

> *"Lakini nina Neno juu yako, ya kwamba umeuacha upendo wako wa kwanza. Basi, kumbuka ni wapi ulikoanguka; ukatubu."*

Ufunuo 2:4-5.

Kanisa lilikuwa katika wakati huo wa kwanza tayari ni "mwanamke aliyeanguka." Kama vile Shetani alivyomfikia Hawa kabla ya Adamu, hata sasa Shetani alikuwa amelidanganya kanisa, bibi-arusi wa Kristo, kabla ya 'karamu ya arusi ya Mwana-Kondoo.' Na ni kitu gani hasa kilichokuwa katikati yake kilichosababisha kuanguka? Ni kitu gani ila Ufu. 2:6, "MATENDO YA WANIKOLAI." Tayari wakati huo wa

kwanza ulikuwa umeacha kulifuata Neno lisiloghoshiwa la Mungu. Waliacha maagizo ya Mungu ya kanisa linalomtegemea Yeye kabisa (linalomtegemea Mungu kabisa kutimiza Neno Lake tangu mwanzo hata mwisho mbali na utawala wa kibinadamu) wakauendea Unikolai, ambao ni kuunda utawala wa kibinadamu kanisani ambayo kama vile serikali zote zifanyavyo, huwaweka watu chini ya sheria. Walifanya vile hasa Israeli ilivyofanya. Waliiendea njia ya utawala wa kibinadamu badala ya Neno na Roho.

Mauti ilikuwa imeingia. Tunajuaje? Je! Sisi hatusikii sauti ya Roho iliyopazwa katika ule wakati wa kwanza kwa ajili ya wote watakaosikia, wakati Yeye akiwaita. *"Yeye ashindaye nitampa kula matunda ya Mti wa Uzima, katika bustani ya Mungu."* Kanisa lilikuwa tayari limekunywa likalewa sana kutoka kwenye mti wa mauti (ama mzabibu wa uongo wa kimadhehebu) ambao mwisho wake ni ziwa la moto. Bali hakuna makerubi wenye panga za moto kuulinda ule Mti wa Uzima sasa. Mungu sasa haondoki katikati ya kanisa kama alivyotoka Edeni. Loo, la, Yeye daima atakuwa katikati ya kanisa Lake mpaka wakati wa mwisho. Na mpaka wakati huo Yeye anawaita wote waje.

Sasa naomba tuwe waangalifu hapa. Ujumbe huu kwa malaika wa kanisa ambalo liko Efeso si ujumbe kwa kanisa halisi la Efeso. Ni ujumbe kwa WAKATI huo. Na wakati huo ulikuwa na mbegu ya kweli ndani yake na mbegu ya upotevu hasa kama ilivyoainishwa kulingana na mfano wa ngano na magugu. Nyakati za kanisa ni shamba, na ndani yake mna ngano na magugu. Kanisa la uongo liliunda madhehebu, wakaunda uongozi wa kanisa kimwili na kulichukua Neno kimwili, na kumpiga vita Mkristo wa kweli.

Magugu daima hustawi kwa nguvu kuliko ngano au mmea mwingine wowote uliopandwa. Kanisa la magugu lilikua upesi sana katika wakati huu wa kwanza. Lakini kanisa la ngano lilikuwa linastawi pia. Hadi kufikia mwisho wa wakati wa kwanza matendo ya Wanikolai yalikuwa yakistawi katika makanisa ya mitaa ya ule mzabibu wa uongo huku yakizidi kujaribu kueneza ushawishi wao kwenye sehemu za mbali zaidi na kundi lao. Ushawishi wake ulionekana kwenye kanisa la kweli kwa maana watu kama mwadhamu Polikapu walikuwa wakijiita maaskofu wakitumia cheo hicho ambacho hakikuwako kulingana na Neno. Pia katika wakati huo, kanisa la kweli lilikuwa limepoteza upendo wake wa kwanza. Upendo huo ulifananishwa na kama upendo wa bibi-arusi na bwana arusi wakati ndoa yao na miaka ya kwanza ya maisha yao ya ndoa. Kulikuweko na kupoa kwa upendo huo mkamilifu na kumwacha Mungu.

Lakini angalia. Ufunuo 2:1 inamweleza Bwana Yesu akiwa katikati ya kanisa Lake na akiwa amewashika wajumbe katika mkono Wake wa kuume. Kwa sababu bibi-arusi huyu ameanguka, kwa sababu kanisa lililounda shirika sasa ni mchanganyiko wa kweli na uongo, Yeye haliachi. Ni Lake.

Na kulingana na Warumi 14:7-9 hiyo ni kweli kabisa.

> *"Kwa maana hakuna mmoja wetu aishiye kwa nafsi yake, wala hakuna mtu anayejifia nafsi yake.*
>
> *"Kwa maana kama tukiishi, twaishi kwa Bwana, na kama tukifa, twafa kwa Bwana; basi kama tukiishi au kama tukifa, tu mali ya Bwana."*
>
> *Kwa maana Kristo alikufa akafufuka, akawa hai tena na kwa sababu hii, awamiliki waliokufa na walio hai pia.*"

Msalabani aliununua ulimwengu MZIMA wa watu. Wao ni Wake. Yeye ni Bwana wa walio hai na waliokufa. (Kwa habari ya umiliki, SI uhusiano.) Naye anatembea katikati ya kundi hilo ambalo lina uhai na mauti ndani yake.

Kile kilichopandwa katika wakati wa kwanza kitakua katika wakati wa pili na katika nyakati nyingine zote mpaka kitakapofikia kupevuka na kuvunwa. Hivyo basi katika Wakati wa Smirna tunatarajia kupanuka na mwangaza wa historia ya shirika la kanisa kupitia ufunuo wa Roho.

Katika wakati huu chuki ya mzabibu wa uongo huongezeka. Mnaona, (aya ya 9) wamejitenga na kundi la walio wa kweli. Walitoka kwao. Walikuwa waongo. Walijiita jina lisilo lao. Lakini je! Mungu aliwaangamiza? La. "Waacheni na wote wawili wataenda kwenye mavuno."

"Lakini Bwana wanapaswa kuangamizwa kwa kuwa wanawaangamiza watu Wako. Wanawaua."

"La, waache. Lakini kwa Bibi-arusi Wangu nasema, 'Uwe mwaminifu hata mauti. Nipendeni hata zaidi. '"

Tunapata kujua waziwazi kabisa ya kwamba mzabibu huu wa uongo ni mzabibu wa Shetani. Kukusanyika kwao ni kwake (Shetani). Wanakutana katika Jina la Mungu na kusema uongo kwamba wao ni wa Kristo. Wanahubiri, wanafundisha, wanabatiza, wanaabudu, wanashiriki katika matendo ya ibada mbali mbali zilizopewa kanisa na Kristo, hata hivyo wao si wa Mungu. Lakini kwa kuwa wao wanasema ni wa Mungu, Mungu atawachukulia kwamba wanahusika na katika kila wakati Yeye anaongea habari zao na kuzungumza nao. Wanatukumbusha hasa juu ya Balaamu. Alikuwa na ofisi ya kinabii. Yeye alijua njia sahihi ya kumkaribia Mungu kama ilivyodhihirishwa katika dhabihu ya wanyama walio safi. Lakini yeye

hakuwa NABII wa kweli WA NENO kwa maana wakati Mungu alipomwambia asiende kumtukuza Balaki kwa uwepo wake yeye alijitahidi kwenda hata hivyo kwa maana alikuwa akiongozwa na tamaa yake ya dhahabu na heshima. Kwa hiyo Mungu akamwacha aende. Mapenzi ya Mungu ya kuruhusia yakachukua mahali pa mapenzi makamilifu ya Mungu kwa sababu ya "tamaa ya moyo" wa Balaamu. Mungu kwa kweli alisema, "Endelea." Je! Mungu alibadilisha nia Yake? La bwana. Mungu alitimiza mapenzi Yake bila ya kujali kwenda kwa Balaamu. Balaamu hakubatilisha mapenzi ya Mungu. Mungu alikuwa na njia Yake haidhuru. Balaamu ndiye aliyepata hasara kwa maana alilipuuza Neno.

Na leo tuna jambo lile lile. Wahubiri wanawake, madhehebu, mafundisho ya uongo, na kadhalika, na watu wakimwabudu Mungu, akijidhihirisha katika Roho nao wakiendelea tu kama alivyofanya Balaamu, wakidai ya kwamba Mungu amenena nao hata wakati ambapo agizo lililopokelewa ni kinyume cha Neno lililofunuliwa. Wala sitakataa ya kwamba Mungu alinena nao. Lakini ilikuwa tu kama wakati aliponena na Balaamu mara ya pili. Kama alivyojua ya kwamba Balaamu alitaka shauku ya moyo wake zaidi ya Neno naye alimpa, hata hivyo wakati huo wote hatimaye akifanya APENDAVYO MWENYEWE; vivyo hivyo leo Mungu huwaambia watu waendelee katika tamaa za mioyo yao wenyewe kwa kuwa wao tayari wamelikataa Neno. LAKINI MAPENZI YA MUNGU YATATENDEKA HAIDHURU. Amina. Natumaini mnaona jambo hili. Halitaondoa tu utata wa mengi ya yale yanayoonekana katika nyakati zote lakini zaidi sana litasaidia katika wakati huu wa mwisho ambao una madhihirisho mengi sana na baraka za nje wakati ambapo kipindi chote kizima kiko kinyume kabisa na 'Mapenzi ya Mungu-Yaliyofunuliwa-kwa-Neno.'

Kama wakati wo wote ulipata kupokea ujumbe wenye nguvu na dhahiri kabisa, wakati huu uliupokea. Ilikuwa, na ni, ile kweli ya Agano la Kale, "Mwana wa mjakazi atamsumbua mwana wa mwuungwana, hata mwana wa mjakazi atafukuzwa atoke." Hilo linatufanya kujua ya kwamba chuki na matukano ya Shetani dhidi ya Wakristo wa kweli yatatolewa kupitia kundi la Wakristo ambao ni wa kawaida na wa uongo, na haya yataongezeka mpaka Mungu atakapong'oa huo mzabibu wa uongo katika mwisho wa Wakati wa Laodikia.

Wakati wa tatu ulifunuliwa na Roho wa unabii ya kwamba kanisa la kilimwengu lingechukua Unikolai kama fundisho. Kule kutenganishwa kwa makasisi na wafuasi kulikua kutoka kwenye kweli ya Biblia ya wazee (wachungaji wa makundi ya mtaa) kutawala kundi hilo kwa Neno, na kuingia kwenye 'matendo ya Wanikolai' ambapo makasisi walijiwekea vyeo kimoja juu ya kingine, kanuni isiyo ya kimaandiko ambayo ilijitokeza kwenye ukasisi uliowaweka makasisi kati ya wanadamu na Mungu, ukiwapa makasisi haki fulani huku wakati wote ukiwanyima wafuasi haki zao walizopewa na Mungu. Huu ulikuwa ni unyang'anyi. Katika wakati huu likawa fundisho. Lilianzishwa kanisani kama neno la Mungu lililohakikishiwa, ambalo kwa kweli halikuwa. Lakini makasisi waliliita Neno la Mungu na kwa hiyo fundisho hilo lilikuwa ni mpinga-Kristo.

Kwa kuwa utawala wa kibinadamu ni siasa tupu za kawaida tu, kanisa lilijiingiza kwenye siasa. Kujiingiza huku kulipewa nafasi na mfalme mtawala wa mabavu aliyeunganisha siasa za kanisa na siasa za serikali na akaanzisha kanisa la uongo (dini ya uongo ya Shetani) kwa kutumia nguvu kama dini ya kweli. Na kupitia kwa amri mbalimbali za watawala mbalimbali tunaona kanisa la uongo likiwa na nguvu za serikali kuuangamiza mzabibu wa kweli hata zaidi.

Inasikitisha kusema mzabibu wa kweli haukuwa na kinga kabisa ya fundisho hili. Kwa kusema hivyo simaanishi kwamba ule mzabibu wa kweli uliwahi kuanzisha mawazo ya Wanikolai kama fundisho. La hasha. Lakini yule mdudu mdogo wa mauti aliendelea kuunyonya mzabibu wa kweli akitumaini kwamba huenda ukaanguka. Hata ndani ya kanisa la kweli, watu ambao Mungu alikuwa amewaita kama waangalizi walikuwa wanachukua cheo hicho kuwa na maana ya madaraka yaliyozidi kidogo tu wajibu kwa mtaa fulani. Haikuwa ule ufahamu dhahiri wa Paulo uliokuwako katika kanisa wakati huu. Kwa maana Paulo alikuwa amesema, "Nao wakamtukuza Mungu ndani yangu." Haidhuru Paulo alikuwa na mamlaka gani, aliwafanya watu wamtazame Mungu ambaye Yeye ana mamlaka yote. Lakini hao makasisi daima walikuwa wakitazamia Uongozi wa Kiungu PAMOJA NA WA KIBINADAMU, na kwa hiyo kutoa heshima mahali ambapo hapakustahili heshima, tunaona ya kwamba kanisa la kweli lilikuwa limetiwa madoadoa ya ubinadamu. Huku Unikolai ukiwa umeimarishwa_uhalifa wa kimitume_wahudumu waliobandikwa na binadamu_wachungaji waliopigiwa kura, na kadhalika., ilikuwa tu ni hatua moja kwa hilo kanisa la uongo kuendelea na kuingia kwenye Ubalaamu. Hatua ya pili ya kuzama kwenye 'fumbo la Shetani' ilikuwa sasa inaendelea kikamilifu.

Hatua hii ya pili ilikuwa ni fundisho la Balaamu, (linaloelezewa katika Ufu. 2:14) ambapo Balaamu alimfundisha Balaki kuwakwanza wana wa Israeli kwa 'mkutano wa muungano'. Huko wageni wangefanya mambo mawili zaidi kinyume cha Neno la Mungu. Mtakumbuka ya kwamba Balaki alihitaji msaada kuudumisha ufalme wake. Akamwita mtu aliyekuwa na nguvu sana kiroho katika siku zake, Balaamu. Balaamu alitoa ushauri uliowatega na kuwaangamiza Israeli. Ilikuwa, kwanza kabisa, kupendekeza ya kwamba wote wakusanyike na kuzungumza kumaliza mambo, na wale pamoja na kunyosha mambo. Baada ya yote, kufahamiana kunasaidia sana. Mara ukitekeleza jambo hilo unaweza kuendelea mbele. Hatua inayofuata ingekuwa ni kuabudu pamoja, na bila shaka, msukumo mdogo kutoka kwa mwenyeji kwa kawaida huwafanya wageni waende mbali zaidi kuliko walivyokusudia. Sasa hilo halikutukia tu nyuma kule kwa kanisa la Mungu la Agano la Kale bali lilitukia kwa kanisa la Agano Jipya, kwa maana kulikuwako na

mfalme, ambaye kama Balaki alihitaji msaada kuulinda ufalme wake.

Kwa hiyo Konstantino akaalika Mkristo wa jina, Kanisa la Kwanza la Kikristo la Rumi, limsaidie kuwafanya Wakristo wamuunge mkono, kwa maana walikuwa ni kundi kubwa sana. Matokeo yalikuwa Baraza la Nikea la 325. Hapo Wakristo, wa kweli na wa kawaida, walikusanyika pamoja kwa mwaliko wa Konstantino. Wakristo wa kweli hawakuwa na shughuli hata kwenda kwenye mkutano. Licha ya yote aliyoweza kufanya Konstantino kuwaunganisha wote, waamini halisi walijua hapo hawakuwa mahali pao na wakaondoka. Lakini kwa wale waliobaki, Konstantino aliwapa mali kutoka katika hazina ya serikali pamoja na nguvu za kisiasa na za kimwili. Watu wakaingizwa katika ibada za sanamu na mizimu, kwani sanamu zenye majina ya watakatifu ziliwekwa katika majengo na watu wakafundishwa kuwasiliana na mizimu, ama kuwaomba dua watakatifu ambalo si jambo lingine ila ibada ya mizimu. Badala ya chakula ambacho mwanadamu anahitaji kweli, yaani Neno la Mungu, walipewa kanuni za imani, na mafundisho ya sharti na ibada za dini ambazo pia zililazimishwa na serikali, na zaidi ya yote walipewa miungu mitatu na jina lenye sehemu tatu za yule Mungu Mmoja wa Kweli, na ubatizo wa maji katika Jina Lake Bwana Yesu Kristo ukabadilishwa na ubatizo wa kipagani wa vyeo vitatu.

Waamini halisi hawakupaswa kwenda kule. Walikuwa tayari wamepoteza kweli nyingi, na sasa wao, pia, watapoteza ufahamu wa Uungu na kubadilisha majina kwa vyeo katika ubatizo wa maji.

Sasa angalia fundisho hili la Balaamu kwa makini sana. Angalia zaidi ya yote, ya kwamba ni njama za makusudi za makasisi wapotovu kuwafunga watu kwao, kwa kuwaongoza watu makusudi katika dhambi ya kutokuamini. Fundisho la Wanikolai lilikuwa ni upotovu wa makasisi walipokuwa wakitafuta nguvu za kisiasa miongoni mwao wenyewe, ambapo Ubalaamu ni kuwatiisha watu chini ya utaratibu wao wa kanuni za imani na ibada kusudi wapate kuwashikilia. Sasa angalia jambo hili kwa makini. Ni kitu gani kilichowafungia watu kwenye kanisa la kawaida na hivyo kuwaangamiza? Ilikuwa ni kanuni za imani na mafundisho ya sharti yaliyoundwa katika kanuni za kanisa. Ilikuwa ni fundisho la Kanisa Katoliki la Kirumi. Hawakupewa chakula cha kweli, Neno. Walipewa chakula kilichotokana na ibada za sanamu, ule upagani wa Kibabeli uliofungwa katika maneno na majina ya Kikristo.

Na roho ile ile na fundisho lilo hilo liko moja kwa moja miongoni mwa Waprotestanti wote na linaitwa DHEHEBU. Unikolai ni Udhehebu, kuufanya uongozi wa kanisa kuwa wa kibinadamu, na hivyo kumwondoa Roho Mtakatifu. Ule Balaamu ni udhehebu ambao unachukua mwongozo wa kanisa badala ya Biblia. Na moja kwa moja mpaka saa hii, wengi wa watu wa Mungu wamenaswa katika mtego wa madhehebu na Mungu anawalilia, “Tokeni kwake watu Wangu, msije mkashiriki dhambi zake, wala msipokee mapigo yake.” Mnaona wao ni wajinga. Lakini kama unyakuo ukitukia wakati huu, ujinga haungekuwa mahakama ya kukata rufaa kutokana na hukumu ya Mungu kwa kuwa katika makundi mabaya.

Makasisi kujiwekea utaratibu wa cheo kimoja juu ya kingine mpaka hatimaye wanaongozwa na rais ni dhihirisho la roho ya mpinga-Kristo, haidhuru linaonekana ni jambo zuri na ni muhimu jinsi gani. Si kitu ila hoja za kibinadamu zikichukua mahali pa Neno. Na mtu ye yote aliye katika utaratibu wa madhehebu yuko moja kwa moja katikati ya utaratibu wa mpinga-Kristo. Sasa hebu niseme jambo hili na kulifanya dhahiri sana. MIMI SIWAPINGI WATU. MIMI NAPINGA MFUMO.

Kukiwa muungano wa serikali na kanisa jukwaa limekwisha andaliwa kwa zile Zama za Giza. Na kwa kweli kwa miaka kama elfu moja kanisa liliingia katika kilindi cha giza, likijua mafumbo ya Shetani. Wakati watu wo wote wa dini wanaposhikilia Unikolai na Ubalaamu, na kuungwa mkono na nguvu za kisiasa, za kifedha na za kimwili kuna upande mmoja tu wanaoweza kwenda. Uelekeo huo unaingia moja kwa moja kwenye fundisho la Yezebeli.

Sasa kwa nini tunasema jambo hili? Kwa sababu kama tulivyosema katika somo la wakati wa nne ya kwamba Yezebeli alikuwa Msidonia, binti wa Etibaali aliyekuwa kuhani mfalme wa Astarte. Yeye alikuwa muuaji. Mwanamke huyu aliolewa na Ahabu (Mfalme wa Israeli) kwa manufaa ya kisiasa. Ndipo alipotwaa mamlaka juu ya dini ya watu na akawaua Walawi, na kujenga mahekalu ambamo aliwafanya watu wamwabudu Astarte (Vinasi) na Baali (mungu Jua). Aliunda mafundisho na kuwafanya makuhani wake wafundishe, nao wakawafanya watu wakubali.

Hapo unaweza kuona vile kanisa la kawaida lilivyokuwa katika zile Nyakati za Giza. Waliacha Neno la Mungu kabisa isipokuwa kwa majina na vyeo vya Uungu na kanuni chache za Maandiko. Walipindisha kile walichotoa katika Biblia kwa kubadilisha maana yake. Chama chao cha maaskofu, nk., kiliandika vitabu vingi, mapapa wao walijitangaza kwamba hawawezi kukosea na wakasema walipokea ufunuo kutoka kwa Mungu na kunena kama Mungu kwa watu. Haya yote walifundishwa makuhani ambao kwa hofu waliwafanya watu wayaamini. Kukataa ilikuwa ni mauti ama kutengwa na kanisa ambayo ingekuwa mbaya kuliko mauti. Sasa ilikuwa ni kanisa lenye sauti iliyoyakinishwa ambalo lilitwaa mamlaka, na likiwa limeenda wazimu kwa nguvu walizokuwa nazo walikunywa damu ya mashahidi mpaka Wakristo wa kweli walikuwa wameangamizwa karibu wote kabisa na karibu hakukuweko na Neno lililosalia, na madhihirisho haba sana ya Roho Mtakatifu. Lakini mzabibu wa kweli ulijitahidi na kuishi. Mungu alikuwa mwaminifu kwa kundi hilo dogo na mbali na yale Rumi ingefanya na miili yao, Rumi haingeweza kuiua Roho iliyokuwa ndani yao, na

nuru ya ile Kweli ikaendelea kuangaza, ikiungwa mkono na Roho Mtakatifu na nguvu.

Hapa ni mahali pazuri pa kufanyia uchunguzi unaotoa mwanga. Angalia. Matendo na mafundisho ya Wanikolai, fundisho la Balaamu, na fundisho la nabii mke wa uongo, Yezebeli, havifanyi roho tatu ama kufanya kanuni tatu za kiroho. Hivi vitatu si cho chote ila ni madhihirisho mbalimbali ya roho yule yule anapoenda kutoka kilindi kimoja kuingia kingine. Yote hayo ni, roho ya mpinga-Kristo ya kimadhehebu katika hatua zake tatu mbalimbali. Mara makasisi walipojitenga na kujiwekea utaratibu waliwakandamiza watu kwa kuwaongoza katika madhehebu, na kuwafunga humo pia. Madhehebu haya yalitegemea kanuni za imani na fundisho la sharti ambalo waliwafundisha watu badala ya Neno safi la Mungu.

Utaratibu wa dini na sherehe za kidini vilizidi kupewa nafasi katika ibada, na punde utaratibu huu wote mzima ulikuwa wenye nguvu ya kivita na ya ibilisi ambayo ilifanya juhudi zote kutawala kila mtu kwa ushawishi wa maneno ama kwa kutumia nguvu kikweli kweli. Utaratibu huu ulipata nguvu zake kutoka kwa unabii wake mwenyewe wa uongo wala si Neno la Mungu. Ulikuwa sasa wa kipinga-Kristo kabisa ingawa ulikuja katika Jina la Kristo.

Baada ya kile kilichoonekana kama wakati usio na mwisho ambapo Kweli haina budi kufa, watu walianza kupinga upotovu wa Kanisa Katoliki la Kirumi, kwa maana huwezi kuwazia hata kidogo kabisa kabisa kwamba Mungu angeweza kuwemo katika fundisho kama hilo ama mwenendo wa jinsi hiyo. Upinzani huu aidha ulipuuzwa kisha ukafa kutokana na kushindwa kuwaamsha watu, ama ulikomeshwa na Rumi. Lakini basi, Mungu katika neema Yake kuu alimtuma mjumbe jina lake Martin Luther kuanzisha matengenezo. Alifanya kazi katika mazingira ambapo Kanisa Katoliki la Kirumi lilikuwa limepewa kamba nyingi sana hivi kwamba lilikuwa karibu kujinyonga. Kwa hiyo wakati Luther alipohubiri kuhesabiwa haki kwa imani mzabibu wa kweli kwa mara ya kwanza katika karne nyingi ulianza kukua kwa ukarimu.

Kama vile kanisa la uongo lilivyokuwa limetumia nguvu za serikali kuliunga mkono, sasa nguvu za serikali zilianza kumiminika kulipinga. Na hapa ndipo Luther alipofanya kosa lake, na waamini wa kweli walifanya kosa lao. Waliruhusu serikali kuwapa ruzuku. Kwa hiyo wakati huu haukupiga hatua kubwa sana kwenye Neno. Mungu ashukuriwe kwamba lilifika umbali liliokwenda, lakini kwa sababu liliegemea zaidi sana kwenye nguvu za kisiasa, wakati huu uliishia kwenye kuunda madhehebu, na kundi lili hili ambalo katika kizazi cha Luther lilikuwa limekatika kutoka kwenye mzabibu wa uongo, sasa likigeuka na kurudi kuwa binti wa kahaba kwa maana liliingia moja kwa moja katika Unikolai na Ubalaamu. Wakati huu ulikuwa na vikundi vingi vilivyofarakana ndani yake, na ili kuthibitisha jinsi walivyokuwa mbali na mzao wa kweli ni kusoma tu historia na kuona jinsi walivyotesana, hata kufikia kuuana wakati mwingine. Lakini kulikuweko na majina machache miongoni mwao, kama vile ilivyo sikuzote katika kila wakati.

Tunafurahi katika wakati huu kwa ajili ya jambo hili moja. Matengenezo yalikuwa yameanza. Haikuwa ufufuo bali matengenezo. Wala haikuwa ni kurejeshwa. Lakini ile chembe ya ngano iliyokuwa imekufa pale Nikea na kuoza katika Zama za Giza, sasa ilitoa chipukizi la kweli ikionyesha ya kwamba kwenye siku za baadaye, mwishoni mwa Wakati wa Laodikia, kabla tu ya Yesu kuja, kanisa litarudi kuwa Bibi-arusi Chembe ya Ngano tena ambapo magugu nayo yangevunwa na kuchomwa katika ziwa la moto.

Kwa kuwa wakati ule wa tano ulikuwa umesababisha kusambazwa sana kwa Neno kwa njia ya uchapishaji, wakati wa sita ulifanya haraka kutumia nafasi hiyo. Wakati huu ulikuwa ndio hatua ya pili ya kule kurejeshwa na kama tulivyokwisha kusema ulikuwa ni wakati wa kishada. Elimu ilijaa tele. Huu ulikuwa ni wakati wa wasomi waliompenda Mungu na kumtumikia. Wamishenari walifurika na Neno likaenea kote ulimwenguni. Ulikuwa ni wakati wa upendano wa ndugu. Ulikuwa ni wakati wa mlango uliofunguliwa. Ulikuwa ni wakati wa mwisho uliodumu muda mrefu, na baada yake Wakati wa Laodikia ungekuja ambao ungekuwa mfupi.

Mzabibu wa kweli ulikua katika wakati huu kuliko wakati mwingine wo wote wakati mtu anapofikiria kuhusu idadi ya nyumbani na katika nchi za ng'ambo. Wakati huu uliwaleta watu watakatifu mbele. Mzabibu wa kweli ulienea na mzabibu wa uongo ukapungua. Kila mahali mzabibu wa kweli ulipoenda Mungu alitoa nuru na uzima na furaha. Mzabibu wa uongo ulidhihirishwa kile ulichokuwa: giza, taabu, umaskini, ujinga na mauti. Na kama vile mzabibu wa uongo katika siku zake za mamlaka usingeweza kuua mzabibu wa kweli, wala mzabibu wa kweli sasa haukuweza kuurudisha mzabibu wa uongo kwa Yesu Kristo. Lakini ule mzabibu wa uongo ulijiimarisha, ukingojea sehemu ya mwisho ya wakati wa mwisho wakati ambapo utawarudisha wote kwake ila lile kundi ambalo ndilo mzabibu uliochaguliwa na wa kweli wa Mungu.

Lakini jinsi wakati huu unavyotufanya tujisikie kuhuzunika tunapotambua ya kwamba kila ufufuo mkuu wa Mungu (na kulikuweko na nyingi) ulipuuza kutupilia mbali fundisho la Wanikolai kwa maana fufuo zote ziliunda madhehebu kisha zikafa. Ndipo wakaunda madhehebu wapate kuwashikilia waliokufa kiroho katika malisho yasiyo na chakula. Hawakuwa na habari hata kidogo na jambo hilo, lakini kila kundi liliambukizwa kosa lilo hilo, na wakati moto wa ufufuo ulipofifia, madhehebu yalichukua mamlaka na watu wakawa madhehebu. Walikuwa ni Wakristo wa jina tu ingawa kila kundi lilidai kwa uhakika ule ule kama Kanisa Katoliki la Kirumi ya kwamba wao walikuwa wako sahihi na hao wengine wote wako makosani. Jukwaa

kweli lilikuwa limeandaliwa kwa ajili ya hao mabinti kurudi nyumbani katika wakati wa mwisho, kurudi Rumi, chini ya mama kuku.

Na kwa hiyo tukafikia wakati wa mwisho: Wakati wa Laodikia. Huo ndio wakati wetu. Tunajua ni wakati wa mwisho kwa kuwa Wayahudi wamerudi Palestina. Haidhuru walifikaje kule; wako pale. Na huu ni wakati wa mavuno. Lakini kabla mavuno hayajakuwako lazima kuwe na kukomaa, kukomaa kwa mizabibu yote miwili.

Wakati wa Kiluteri ulikuwa ni majira ya kuchipua. Wakati wa Wesley ulikuwa majira ya kiangazi ya kukua. Wakati wa Laodikia ni wakati wa mavuno wa kukusanya magugu kwa ajili ya kufungwa na kuchomwa moto; na kuweka ngano ghalani kwa ajili ya Bwana.

Wakati wa mavuno. Wakati wa mavuno. Je! uliambua kwamba katika wakati wa mavuno, ingawa kuiva kunaharakisha dhahiri sana, vivyo hivyo kukua kunapungua mpaka hakuna kukua tena? Je hilo silo kwa kweli tunaloona hivi sasa? Ule mzabibu wa uongo unapoteza umati wa watu kwa Wakomunisti na imani za aina nyingi. Idadi yake haiongezeki kama ambavyo ungetaka sisi tuwazie. Kuwashikilia kwake watu si kama vile ilivyokuwa, na mara nyingi sana kwenda kanisani ni onyesho tu. Na mzabibu wa kweli? Vipi kuhusu yeye? Je! Unakua? Iko wapi ile idadi kubwa sana inayoendelea kuja kwenye ufufuo na kuitikia wito wa madhabahuni? Je! wengi wao sio wanaoongozwa na mwamsho tu, ama walio na shauku ya jambo fulani la kimwili mbali na shauku ya jambo ambalo ni la Kiroho kweli? Je! siku hii siyo kama siku ambayo Nuhu aliingia safinani, nao mlango ukafungwa, lakini hata hivyo Mungu akangojea katika hukumu siku saba? Hakuna mtu aliyemgeukia Mungu hasa katika siku hizo za kimya.

Na hata hivyo ni wakati wa mavuno. Hapo basi lazima waje katika wakati huu wale ambao wataifikisha ngano na magugu kwenye ukomavu. Magugu tayari yanakomaa haraka sana chini ya waalimu wapotovu wanaowaondoa watu kwenye Neno. Lakini ngano pia haina budi kukomaa. Na, Mungu anamtuma kwake Nabii-Mjumbe akiwa na huduma iliyothibitishwa kusudi akubaliwe na wateule. Watamsikia kama vile kanisa la kwanza lilivyomsikia Paulo, naye bibiarusi atakomaa katika Neno mpaka hapo atakapokuwa Bibiarusi Neno kazi kubwa zitatendeka ndani yake ambazo daima zinaambatana na Neno lisiloghoshiwa na imani.

Makundi ya makanisa ya uongo yataungana katika baraza la makanisa ulimwenguni. Baraza hili la makanisa ndilo SANAMU ILIYOTENGENEZEWA MNYAMA.

Ufunuo 13:11-18,

> *"Kisha nikaona mnyama mwingine, akipanda juu kutoka katika nchi; naye alikuwa na pembe mbili mfano wa MwanaKondoo, akanena kama joka.*
>
> *Naye atumia uwezo wote wa mnyama yule wa kwanza mbele yake, naye aifanya dunia na wote wakaao ndani yake wamsujudie mnyama wa kwanza, ambaye jeraha lake la mauti lilipona.*
>
> *Naye afanya ishara kubwa, hata kufanya moto kushuka kutoka mbinguni uje juu ya nchi mbele ya wanadamu.*
>
> *Naye awakosesha wale wakaao juu ya nchi, kwa ishara zile alizopewa kuzifanya mbele ya huyo mnyama, akiwaambia wakaao juu ya nchi kumfanyia sanamu yule mnyama, aliyekuwa na jeraha la upanga naye akaishi.*
>
> *Akapewa kutia pumzi katika ile sanamu ya mnyama, hata ile sanamu ya mnyama inene, na kuwafanya hao wote wasioisujudu sanamu ya mnyama wauawe.*
>
> *Naye awafanya wote, wadogo kwa wakubwa, na matajiri kwa maskini, na walio huru kwa watumwa, watiwe chapa katika mkono wao wa kuume, au katika vipaji vya nyuso zao;*
>
> *Tena kwamba mtu awaye yote asiweze kununua wala kuuza, isipokuwa ana chapa ile, au, jina la mnyama yule, au hesabu ya jina lake.*
>
> *Hapa ndipo penye hekima. Yeye aliye na akili, na aihesabu hesabu ya mnyama huyo; maana ni hesabu ya kibinadamu; na hesabu yake ni mia sita, sitini na sita."*

Sasa kumbuka, Dola ya Kipagani ya Rumi ndiyo iliyoanguka kwa upanga. Lakini iliponywa pigo lake la mauti wakati ilipoungana na kanisa la kawaida la Kikristo la Rumi na kuchanganya upagani na Ukristo, na hapo ikawa Dola Takatifu ya Kirumi ambayo ilikuwa idumu mpaka Yesu atakapokuja na aiangamize. Lakini Rumi haiko peke yake. Binti zake wako moja kwa moja pamoja naye naye atachukua mamlaka yenye amri zote kwa njia ya Baraza la Makanisa Ulimwenguni.

Hili linaweza kuonekana kama jambo la uongo kwa wengine lakini kwa kweli liko dhahiri sana kwa wote kuona kwa sababu sasa hivi makanisa yanamiliki siasa na katika wakati unaofaa yatadhihirisha

barabara jinsi utawala huo ulivyo na nguvu. Shughuli hizi za ekumeni zitaishia na Rumi kama kiongozi wake hata ingawa watu hawakuliona jinsi hiyo. Hii ni kwa sababu katika Ufunuo 17:3-6 inasema kwamba yule kahaba, Babeli ya siri ameketi juu ya mnyama. Yeye anaongoza ile himaya ya mwisho, ama ya nne. Kanisa hili la Kirumi linafanya jambo hilo. Huku kanisa la muungano la ulimwengu likiwa chini yake Rumi itakuwa ikitawala, na sanamu hii (muungano wa kanisa) itaitii Rumi kwa maana Rumi inamiliki dhahabu ya ulimwengu.

Hivyo basi watu wote hawana budi kuwa washiriki wa kanisa la muungano la ulimwengu ama watiishwe na hali ya nchi kwa maana hawawezi kununua ama kuuza bila alama ya mnyama mkononi ama kichwani. Alama hii kichwani inamaanisha ya kwamba itawabidi kuamini mafundisho ya hilo shirika la kanisa la ulimwengu ambayo ni utatu, na kadhalika., na ile alama mkononi ambayo maana yake ni kufanya mapenzi ya kanisa la ulimwengu. Kwa nguvu hizi kuu mifumo ya kanisa itamtesa bibi-arusi wa kweli. Sanamu hii itajaribu kumzuia bibi-arusi kuhubiri na kufundisha, na kadhalika. Wahudumu wake watakatazwa kuwapa faraja na kweli watu wanaohitaji. Lakini kabla ya mpinga-Kristo (mtu halisi) kutwaa mamlaka kamili juu ya utaratibu huu wa makanisa ulimwenguni kanisa la kweli litaondolewa hapa ulimwenguni likaishi pamoja na Bwana. Mungu atamnyakua bibi-arusi Wake kwa ajili ya ile Karamu kuu ya Arusi ya Mwana-Kondoo.

Sasa kwa vile sura hii ya mwisho ilitolewa kusudi tuweze kufuatilia yale makanisa mawili na zile roho mbili tangu Pentekoste hadi mwisho wao, tutachukua wakati huu wa mwisho kuonyesha jambo hili katika Wakati wa Laodikia.

Wakati huu ulianza baada tu ya mwanzo wa karne ya ishirini. Kwa kuwa ulikuwa uwe ni wakati ambapo kanisa la kweli lingerudi kuwa bibi-arusi kama alivyokuwa wakati wa Pentekoste, tunajua ya kwamba hapana budi kuwe na kurudishwa kwa zile nguvu kuu. Waamini walihisi jambo hili katika roho zao na wakaanza kumlilia Mungu wapate kumwagiwa kupya kama ilivyokuwa katika karne ya kwanza.

Kitu kilichoonekana kama jibu kilikuja wakati wengi walipoanza kunena kwa lugha na kudhihirisha karama za Roho. Wakati huo iliaminika ya kwamba huku kulikuwa ndio kweli kule KURUDISHWA kulikongojewa kwa muda mrefu. La, haikuwa jambo hilo, kwa maana mvua ya vuli inaweza tu kuja baada ya mvua ya masika ambayo ni mvua ya kuchipusha ama ya KUFUNDISHA. Mvua ya vuli, basi, ni mvua ya KUVUNIA. Hili lingewezaje kuwa ndilo jambo halisi ambapo Mvua ya Kufundisha haikuwa imekuja? NabiiMjumbe aliyekuwa atumwe KUWAFUNDISHA watu na kuigeuza mioyo ya watoto wao iwaelekee baba zao wa Pentekoste hakuwa amekuja bado. Hivyo basi kile kilichodhaniwa kuwa ni kurejezwa na kuhuishwa kwa mwisho hadi kufikia kunyakuliwa hakikuwa kimekuja. Ndani yake kulikuweko na mchanganyiko wa wasio haki wakishiriki baraka za Kiroho na kumdhihirisha Roho Mtakatifu kama vile tulivyodumu kuwaonyesha. Ndani yake pia kulikuweko na nguvu za ibilisi kwa kuwa watu walikuwa chini ya uongozi wa mapepo, lakini hakuna mtu aliyeonekana anajua jambo hilo. Ndipo, ili kuthibitisha ya kwamba halikuwa ni lile jambo lenyewe HALISI, watu hawa (hata kabla ya kizazi cha pili kutokea) waliunda madhehebu, na wakaandika mafundisho yao yasiyo ya kimaandiko na kujijengea maboma yao wenyewe kama kila kundi lingine lo lote lililowatangulia lilivyofanya.

Kumbuka, wakati Yesu alipokuwa duniani vivyo hivyo na Yuda pia alikuwepo. Kila mmoja wao alitokana na roho tofauti, na walipokufa kila mmoja alienda mahali pake. Roho ya Kristo ilirudi baadaye juu ya kanisa la kweli, nayo roho ya Yuda ikarudi juu ya kanisa la uongo.

Ni pale pale katika Ufu. 6:1-8,

> *"Nikaona, na tazama, farasi mweupe, na yeye aliyempanda ana uta, akapewa taji, naye akatoka, ali akishinda tena apate kushinda. Na alipoifungua muhuri ya pili, nikamsikia yule mwenye uhai wa pili akisema, Njoo uone!*
>
> *Akatoka farasi mwingine, mwekundu sana, na yeye aliyempanda alipewa mamlaka kuiondoa amani katika nchi, ili watu wauane, naye akapewa upanga mkubwa.*
>
> *Na alipoifungua muhuri ya tatu, nikamsikia yule wa tatu mwenye uhai akisema, Njoo uone! Nikaona, na tazama, farasi mweusi, na yeye aliyempanda ana mizani mkononi mwake.*
>
> *Nikasikia kama sauti katikati ya hao wenye uhai wanne, ikisema, Kibaba cha ngano kwa nusu rupia, na vibaba vitatu vya shayiri kwa nusu rupia, wala usiyadhuru mafuta wala divai.*
>
> *Na alipoifungua muhuri ya nne, nikasikia sauti ya yule mwenye uhai wa nne akisema, Njoo uone!*
>
> *Nikaona, na tazama, farasi wa rangi ya kijivujivu, na yeye aliyempanda jina lake ni Mauti, na Kuzimu akafuatana naye. Nao wakapewa mamlaka juu ya robo ya nchi, waue kwa upanga na kwa njaa na kwa tauni na kwa hayawani wa nchi."*

Angalia jinsi ambavyo huyo roho wa Yuda alivyorudi kama mpanda farasi mweupe. Alikuwa mweupe. Ni karibu sana na halisi, kama tu vile Yuda alivyokuwa karibu sana na Yesu. Alipewa taji (mpanda farasi mweupe). Vipi? Roho huyo alikuwa sasa ndani ya kiongozi wa utaratibu huo wa Uanikolai na alikuwa papa aliyetiwa taji yenye sehemu tatu ambaye aliketi kama Mungu katika hekalu lake, akijiita mwenyewe aliye badala ya Kristo. Kama aliye badala ya Kristo inamaanisha 'badala ya Kristo' ama 'mahali pa' ama 'kwa niaba ya Mungu' basi papa alikuwa akijiita Roho Mtakatifu, ama anamwondoa Roho Mtakatifu, akitenda badala Yake. Hiyo ilikuwa ni roho ya Yuda ndani yake ikifanya hivyo. Angalia jinsi alivyoshinda_naye akatoka ali akishinda tena apate kushinda. Kristo hakufanya hivyo. Wale tu waliomjia walikuwa tayari wamechaguliwa tangu zamani na Baba. Na kwa hiyo huyo roho akaendelea na kuendelea na siku moja itafanyika mwili kweli ndani ya mtu ambaye ataongoza Baraza la Makanisa ulimwenguni, kama tu vile tulivyokuwa tukisema. Na kwa dhahabu yake (kumbuka Yuda ndiye aliyekuwa na ule mfuko) atautawala ulimwengu wote, na utaratibu huo wa mpingaKristo utamiliki kila kitu na kujaribu kumtawala kila mtu. Lakini Yesu atarudi na kuwaangamiza wote kwa nuru ya kuja Kwake. Na mwisho wao utakuwa ni ziwa la moto.

Lakini vipi kuhusu uzao wa kweli? Itatendeka kama tu tulivyosema. Watu wa Mungu wanafanywa tayari kwa Neno la Kweli kutoka kwa mjumbe wa wakati huu. Ndani ya bibi-arusi utakuweko utimilifu wa Pentekoste kwa maana Roho atawarudisha watu moja kwa moja mahali walipokuwa hapo mwanzo. Hiyo ni "Bwana asema hivi."

Ni "BWANA asema hivi" kwa kuwa hivyo ndivyo Yoeli 2:23- 26 inavyosema,

> *"Furahini, basi, enyi wana wa Sayuni, mkamfurahie Bwana, Mungu wenu; kwa kuwa Yeye amewapa ninyi mvua ya masika, kwa kipimo cha haki, Naye atawanyeshea mvua, mvua ya masika, na mvua ya vuli, katika mwezi wa kwanza.*
>
> *Na sakafu za kupepetea zitajaa ngano, na mashinikizo yatafurika kwa divai na mafuta.*
>
> *Nami nitawarudishia hiyo miaka iliyoliwa na nzige, na parare, na madumadu, na tunutu, jeshi Langu kubwa nililolituma kati yenu.*
>
> *Nanyi mtakula chakula tele na kushiba, na kulihimidi Jina la Bwana, Mungu wenu, aliyewatendea mambo ya ajabu; na watu Wangu hawatatahayari kamwe."*

Sasa inasema Mungu "atarudisha". Wakati wa Luther haukulirejesha kanisa; ulianzisha matengenezo. Wakati wa Wesley haukurejesha. Wakati wa Pentekoste haukurejesha. Lakini Mungu hana budi kurejesha kwa kuwa hawezi kulikana Neno Lake. Huu si ufufuo wa Kanisa; ni "Kurejeshwa". Mungu atalipeleka Kanisa moja kwa moja kwenye Pentekoste ya mwanzo. Sasa angalia katika kifungu cha 25 inaeleza ni kwa nini tunahitaji kurejeshwa. Nzige, parare, madumadu na tunutu wamekula yote ila mizizi na kipande kidogo cha shina. Sasa tunaambiwa ya kwamba wadudu hawa wote ni mdudu mmoja na ni yule yule katika hatua mbalimbali. Hiyo ni kweli. Hao ni roho ya mpinga-Kristo ikidhihirishwa katika mashirika, madhehebu na fundisho la uongo katika nyakati zote. Na maskini mzizi huo mdogo na ubua vitarejeshwa. Mungu hatapanda Kanisa jipya, bali atarudisha upandaji Wake wa asili kwenye mbegu ya asili. Yeye anafanya jambo hilo kama lilivyoelezwa katika aya ya 23, kwa mafundisho, ama mvua ya "masika." Inayofuatia itakuwa mvua ya mavuno ama imani ya kunyakuliwa.

Hivyo basi katika wakati uu huu tuko katika kutimizwa kabisa kwa Mt. 24:24 *"wapate kuwapoteza, kama yamkini, hata walio wateule."* Na ni nani atakayejaribu kuwapoteza walio wateule? Ni ajabu, ni roho wa mpinga-Kristo katika "waliopakwa mafuta wa uongo" wa siku hii ya mwisho. Hawa waongo tayari wamekwisha kuja katika "Jina la Yesu" wakidai kwamba wametiwa mafuta na Mungu kwa ajili ya siku ya mwisho. Wao ni Masihi wa uongo (waliotiwa mafuta). Wanadai ya kwamba wao ni manabii. Lakini wao ni mmoja na Neno? Kamwe. Wao wameliongeza ama walilipunguza. Hakuna mtu anayekana ya kwamba Roho wa Mungu akijidhihirisha katika karama yuko juu yao. Lakini kama vile Balaamu wote wana mipango yao, wanaomba pesa, wanatumia karama, lakini wanalikana Neno ama wanaliepa kwa ajili ya hofu kwamba huenda upinzani ungeweza kukatiza nafasi zao za kunufaika zaidi. Hata hivyo wao wanahubiri wokovu na ukombozi kupitia nguvu za Mungu, kama tu Yuda, alivyokuwa na huduma aliyopewa na Kristo. Lakini kwa sababu wao ni wa uzao mbaya, basi wanaongozwa na pepo mchafu.

Wa kidini? Jamani! Wanawashinda walio wateule katika bidii na juhudi, lakini ni ya Laodikia, si ya Kristo, kwa maana wanatafuta kupata makundi makubwa, maazimio makubwa na ishara za kustaajabisha miongoni mwao. Wao wanahubiri kuja kwa Kristo kwa mara ya pili, lakini wanakana kuja kwa nabii-mjumbe, ingawa katika nguvu na ishara na ufunuo wa kweli anawashinda wote. Naam, roho hii ya uongo ambayo katika siku za mwisho inafanana sana na ya kweli, inaweza kutambuliwa tu kwa jinsi anavyoenda mbali na Neno, na kila wakati inaposhikwa kuwa iko kinyume cha Neno, inarukia hoja moja ambayo tayari tumekwisha onyesha kwamba ni ya uongo: "Tunapata matokeo, sivyo? Hatuna budi kuwa wa Mungu."

Sasa kabla hatujafunga, ninataka kuleta wazo hili. Muda huo wote tumekuwa tukizungumzia juu ya Chembe ya Ngano ikizikwa, kisha inatoa machipukizi mawili, kisha kishada, halafu suke la kweli. Jambo hili

linaweza kuwafanya wengine washangae iwapo tulisema ya kwamba Waluteri hawakuwa na Roho Mtakatifu kwa sababu tu wao walifundisha kimsingi tu kuhesabiwa haki. Inaweza kuwafanya wengine waduwae kuhusu Wamethodisti, nk. La bwana, hatusemi hivyo. Hatuzungumzii juu ya watu binafsi ama watu, bali ni kuhusu ule WAKATI. Luther alikuwa na Roho wa Mungu, lakini wakati wake haukuwa ni wakati wa kurudishwa kukamilfu kwa kumwagwa kwingine kama ilivyokuwa hapo mwanzo. Ilikuwa ni vivyo vivyo kwa Wesley, Booth, Knox, Whitefield, Brainard, Jonathan Edwards, Meuller, nk. Hakika walikuwa wamejaa Roho Mtakatifu. Naam, hakika walikuwa. Lakini wakati ambao kila mmoja aliishi haukuwa wakati wa kurejeshwa, wala hapakuwepo na wakati mwingine wo wote ila wakati huu wa mwisho, wakati wa giza kabisa katika ukengeufu. Huu ni wakati wa ukengeufu, na huu ni wakati wa kurejeshwa, ni wakati wa duara iliyokamilika. Kwa hili, yote yamekwisha.

Kwa hiyo tunamalizia zile Nyakati Saba za Kanisa, tukisema tu yale Roho aliyosema kwa kila wakati, "Yeye aliye na sikio na asikie yale Roho anayoyaambia makanisa."

Ninaamini kwa uaminifu ya kwamba Roho wa Mungu amekuwa akinena nasi, si tu kutufundisha kweli za zile nyakati, bali Yeye amekuwa akiishughulikia mioyo kwa uaminifu kwamba ipate kumgeukia Yeye. Hiyo ndiyo sababu ya kuhubiri kote na kufundisha, kwa maana ni katika kuhubiri na kufundisha kwa Neno ambapo kondoo huisikia sauti ya Mungu na kumfuata Yeye.

Kamwe siwaletei watu ujumbe kusudi wanifuate, ama wajiunge na kanisa langu, ama waanzishe ushirika fulani na madhehebu. Sijawahi kufanya hivyo kamwe na sitafanya hivyo sasa. Sivutiwi na mambo hayo, bali ninavutiwa na mambo ya Mungu pamoja na watu, na kama nnaweza kutimiza jambo moja tu nitaridhika. Jambo hilo moja ni kuona uhusiano wa kweli wa kiroho kati ya Mungu na watu umeimarishwa, ambapo watu wanakuwa viumbe vipya katika Kristo, wamejazwa na Roho Wake na kuishi kulingana na Neno Lake. Ningewaalika, ningewasihi na kuwaonya watu wote waisikie sauti Yake wakati huu, na kuyatoa maisha yenu kabisa Kwake, yaani kama vile ninavyotumaini moyoni mwangu kwamba nimempa Yeye yote niliyo nayo. Mungu awabariki, na kuja Kwake kuufurahishe moyo wako.

www.messagehub.info

Mahubiri Na
William Marrion Branham
"... katika siku za sauti ..." Ufu. 10:7